

MWALIMU, JUA HAKI ZAKO NA WAJIBIKA IPASAVYO **KATIKA UTUMISHI WAKO, HAKUNA ATAKAYEKUGUSA!**

Na: Mwl. Andrew Gilayda
Mbulu DC—MANYARA
Phone No. 0782852082
Email address: gilaydaandrew@gmail.com

Vyama vya wafanyakazi ni vyama vya hiari, hakuna mfanyakazi anayepaswa kulazimishwa kujiunga na chama kimojawapo bila hiari yake mwenyewe. Kada ya ualimu ni kada muhimu sana kwani inahusika na msingi wa taaluma zote duniani. Walimu wanapaswa kulindwa dhidi ya dhuluma yeyote dhidi yao. Viongozi waliopewa dhamana ya kuwasimamia walimu hawapaswi kuwa mbwa mwitu wanaowatafuna walimu! Sidhani kama kuna MKURUGENZI, AFISA UTUMISHI, AFISA ELIMU WA JIJI, MANISPAA, MJI, WILAYA AU KATA, MDHIBITI UBORA WA SHULE, MKUU WA SHULE au mamlaka yoyote inayohusika na usimamizi wa mwalimu inaweza kuingilia uhuru wa mwalimu wa kujiunga na chama chake cha wafanyakazi anachokipenda. Kama kuna maafisa wa aina hiyo, wanavunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema:

Ibara ya 20(1) kwamba, “Kila mtu anastahili kuwa huru bila ya kuathiri sheria za nchi, kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika na kushirikiana na watu wengine, kutoa mawazo hadharani, na hasa zaidi kuanzisha au kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo.”

Ibara ya 20(4) kwamba, “Bila ya kuathiri sheria za nchi zinazohusika, ni marufuku kwa mtu yeyote kulazimishwa kujiunga na chama chochote au cha siasa, kukataliwa kusajiliwa kwa sababu tu ya itikadi au falsafa.”

KWA MAELEZO ZAIDI:

Soma vifungu vifuatavyo vya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini no. 6 ya Mwaka 2004 kwenye ukurasa 4 wa makala haya. Jikomboe, usionewe na kunyanyaswa na **chama chochote cha wafanyakazi ulichopo sasa, au kiongozi yeyote aliyepewa dhamana ya kukusimamia.** Sheria inakuruhusu kuamua hatua yoyote kati ya hatua zifuatazo:

(1) Kusitisha uanachama wako uliopo sasa wakati wowote utakapoamua na kubaki katika ajira yako bila ya kuwa mwanachama wa chama chochote cha wafanyakazi au ukihiarika, unaweza kuendelea kuwa mwanachama wa chama hicho **(Kif. 61(4)(5))**

(2) Kujiunga na chama chochote unachokipenda kati ya vyama vya wafanyakazi vilivyopo. **Kif 9 (1) (a) (b)**. Kwa upande wa walimu wa **TANZANIA BARA**, kwa sasa kuna **vyama viwili** vya walimu vilivyoruhusiwa kuendesha shughuli zake; **CWT ambacho kinakata 2% ya mshahara wako** kama ada ya uanachama na **CHAKUHAWATA ambacho kinakata Tshs. 5,000/= tu**, bila kujali kiwango cha mshahara wako.

(3) Kuanzisha chama kipya cha wafanyakazi baada ya kukidhi vigezo vya kisheria **Kif. 9 (1) (a) (b)**.

MAMBO YA MSINGI YA KISHERIA UNAYOPASWA KUFAHAMU!

- **ILI UTAMBULIKE** kuwa mwanachama wa chama cha wafanyakazi utapaswa kuomba rasmi kuwa mwanachama kwa kujaza fomu ya kisheria ijulikanayo kama **TUF 15 kwa sasa**, ambapo utamwelekeza mwajiri wako kukata ada ya uanachama kwa kuzingatia katiba ya chama chako. **(Rejea Kif. 61 (1)(2)(3)(4))**. Kama utaomba kuwa mwanachama wa **CWT utaidhinisha makato ya 2%** ya mshahara wako kama ada ya uanachama; Kama utaomba kuwa mwanachama wa **CHAKUHAWATA utaidhinisha makato ya Tshs. 5,000/=** kama ada ya uanachama. **Hii ni kwa mujibu wa Katiba za vyama hivyo.**
- **AIDHA** ukiamua kukaa bila kujiunga na chama chochote cha wafanyakazi sheria inakulazimisha kuchangia **ada ya uwakala (Agency Fee)**, na hiyo itakatwa na mwajiri wako moja kwa moja kutoka katika mshahara wako **(Rejea Kanuni ya 37(2) ya Kanuni za sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na 6 ya mwaka 2004)**. Hivyo, inashauriwa kuwa ni bora kuwa mwanachama wa chama cha wafanyakazi, maana makato yanayofanyika kwa wanachama yanafanyika pia kwa wasio wanachama. Hata hivyo, **kwa sasa, ada hiyo ya uwakala imesimamishwa na Kamishna wa Kazi, hadi vyama husika vitakapotekeleza matakwa yaliyoainishwa katika sheria.**
- **HAKUNA** mfanyakazi atakayelazimishwa aidha na chama cha wafanyakazi au na mwajiri yeyote kujiunga na chama cha wafanyakazi. **Ni kosa kisheria kufanya hivyo!! Rejea Kif. 72 (1) na vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapo juu.**
- **KAMA ULISHAKUWA MWANACHAMA** wa chama kimojawapo kati ya **CWT au CHAKUHAWATA**, na unataka kubadilisha maamuzi yako kwa kuhamia chama kingine **uko huru** kisheria kufanya yafuatayo:

- 1) Kusitisha uanachama wako wa awali na kumweleza mwajiri wako kusitisha makato yaliyokuwa yakifanyika awali kwenye mshahara wako. Hapo utatoa taarifa ya siku 30 (mwezi mmoja), kwamba umesitisha uanachama wa chama chako cha wafanyakazi. Taarifa hiyo utaiandika kwa chama chako cha awali na kwa mwajiri wako. **Soma Kifungu cha 61(4)**
- 2) Kumwelekeza mwajiri wako kuingiza makato mapya ya ada ya uanachama wa chama chako kipa kwa kujaza fomu itwayo **"Trade Union Form Na. 15 (TUF.15)"**. Mathalan, utamwelekeza mwajiri aondoe makato ya **CWT ya 2%** kwenye mshahara wako, na kuingiza makato ya **Tshs. 5,000/= ya CHAKUHAWATA**. **Soma Kifungu cha 61(1)(4)**
- 3) Baada ya **siku 30** tangu ulipotoa maelekezo hayo, mwajiri **atalazimika kisheria** kusitisha makato ya awali na kuingiza makato mapya kwa kadri ya maelekezo yako. **(Rejea Kif. 61(5))**. Hilo ni takwa la kisheria! Kumbuka, wewe ndiye mwenye mamlaka na mshahara wako, na si vinginevyo! **Soma Kifungu cha 28 (a) (b)**

✚ HAKUNA MAHALI KATIKA SHERIA PANAPOELEKEZA MWAJIRI KUFANYA MAKATO YA VYAMA VIWILI KATIKA MSHAHARA WA MFANYAKAZI! NI KOSA KISHERIA MWAJIRI KUKATA MSHAHARA WA MFANYAKAZI BILA IDHINI YA MFANYAKAZI HUSIKA AU MAELEKEZO MENGINE YA KISHERIA! (Rejea Kif. 28 (1)(a) (b))

TAARIFA: Walimu si watumishi pekee wenye vyama viwili katika nchi yetu. Kuna pia:

- ✚ Wafanyakazi wa serikali Kuu-vyama vyao ni **RAAWU, THT, TEWUTA n.k**; Watumishi wa Taasisi za Fedha- vyama vyao ni **FIBUCA** na **TIUCO**; Wafanyakazi wa migodini-vyama vyao ni **TAMICO** na **NUMET**, na wengineo.
- ✚ **Wote hao, waajiri wao wanaendelea kutenda haki kwa vyama vyao vyote kwa kuzingatia sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini. Walimu pia wana hiari ya kuchagua kujiunga na chama cha wafanyakazi wanachokitaka kwa mujibu wa sheria!**

NUKUU ZA VIFUNGU VYA SHERIA:

- ✓ **Kif. 9(1)** Mfanyakazi yeyote atakuwa na haki ya:
 - (a) Kuanzisha na kujiunga na chama cha wanyakazi**
 - (b) Kushiriki katika shughuli halali za chama cha wafanyakazi**

 - ✓ **Kif. 28 (1)** Mwajiri haruhusiwi kufanya makato yoyote kutoka katika mshahara wa mfanyakazi isipokuwa kama:
 - (a) Makato hayo ni ya kisheria, yanatokana na makubaliano ya pamoja, maamuzi juu ya mshahara n.k.**
 - (b) Endapo mwajiriwa kwa maandishi amekubali makato kutokana na deni lake.**

 - ✓ **Kif. 61**
 - (1)** Mwajiri atakata ada ya chama cha wafanyakazi kutoka katika mshahara wa mfanyakazi ambaye ameridhia na kumruhusu mwajiri kukata ada hiyo kwa kujaza fomu maalum.
 - (2)** Mwajiri atawakilisha kwa chama fedha za makato hayo ndani ya siku saba baada ya mwisho wa mwezi tangu fedha hizo zikatwe.
 - (3)** Mwajiri atakayeshindwa kutekeleza kuwasilisha makato hayo bila sababu za msingi atalipa riba ya asilimia tano kwa kila siku atakayocheleweshwa
 - (4)** Mfanyakazi anaweza kutengua idhini yake ya kukatwa ada ya chama kwa kutoa taarifa ya maandishi ya mwezi mmoja kwa mwajiri na chama.
 - (5)** Baada ya mwezi mmoja kutimia mwajiri atasitisha makato hayo.
 - (6)** Wakati wa kuwasilisha makato ya ada ya kila mwezi mwajiri ni lazima akipatie chama:
 - (a)** Orodha katika fomu maalum ya majina ya wanachama ambao wamekatwa ada.
 - (b)** Nakala ya kutengua idhini ya kukatwa ada.
- ❖ *Nukuu hizi ni kwa mujibu wa tafsiri ya Kiswahili ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na. 6 ya mwaka 2004 (ELRA)*

MWISHO.